

Salamu kwa Familia za Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb!

Mimi ni msimamizi wa Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb, Bi. Cheryl Watson-Harris.

Ninatumaini kwamba mmeanza vyema Mwaka huu Mpya. Asante kwa ustahimilivu, bidii, uvumilivu, na ujasiri wenu wa kuongoza watoto wetu. Afya na usalama wa wafanyakazi, watoto wetu, na familia zao unaendelea kuwa kipaumbele chetu cha juu.

Wakati wa mkutano wa Bodi ya Elimu uliofanywa usiku uliopita, Januari 11, 2021, nilisema kwamba tutawachelewesha wanafunzi kurudi shuleni. Wanafunzi hawatarudi kwa masomo ya ana kwa ana mnamo Januari 19 kama ilivyopangwa awali. Wafanyakazi wa shule wataendelea kulenga kutekeleza mikakati ya kuwa tayari na kupunguza hatari ambayo ni maelekezo ya CDC ya kusaidia kupunguza hatari na kuenea kwa COVID 19.

Vipaumbele vyetu kwa sasa, kama vinavyokuwa kila wakati, ni huruma badala ya utiifu na kuweza kubadilika kwa urahisi kulingana na hali na uvumilivu.

Uamuzi wa kuchelewesha kufungua tena majengo yetu ya shule kwa wanafunzi ni uamuzi mgumu na ninakuhakikishia tunafanya kila kitu katika uwezo wetu ili kufungua tena. Tutafanya hivyo tu wakati tunaweza kuhakikisha wanafunzi na wafanyakazi wanaweza kurudi salama. Kwa kuongezea uwezo wetu wa kufuatilia mikakati ya kupunguza hatari, viwango vya visa ni kiashiraji kingine ambacho tunazingatia katika mchakato wa kutoa uamuzi. Kulingana na mwongozo kutoka kwa CDC, asilimia 10 au zaidi ya viwango vya visa vinatuweka katika hatari kubwa ya maambukizi. Hadi Jumatatu, viwango vya visa katika DeKalb vilikuwa asilimia 14.7%.

Wakati wa ziara zangu za shule katika wiki hizi mbili zilizopita, nilifurahi kuona waalimu wengi sana walioweza kurudi. Walitoa ahadi yao kwa wanafunzi wetu na wamefurahi kuhusu kurudi kwa majengo ya shule. Sina maneno ya kutosha ya kutoa shukrani zangu kwa ahadi yao kwa DCSD. Kwa kuongezea, tunaendelea kuwaunga mkono waalimu na wafanyakazi wetu wa shule ambao wameomba buraa za ugumu.

Tunapokuwa tukijiandaa kwa masomo ya ana kwa ana baadaye, timu yetu ya Operations itaendelea kutekeleza ukaguzi muhimu wa maandalizi ya shule, ambao unajumuisha kutathmini:

- Bidhaa za Kujikinga (PPE) na Bidhaa za Usafi
- Usambazaji wa Bidhaa za Usafi na Taratibu
- Kukaa Mbali na Wengine na Kupanga Nafasi
- Kupata Maji

- Mabomba na Mifumo ya HVAC
- Ishara za Usalama za COVID-19 shuleni

Tunataka kuhakikisha kwamba wafanyakazi na wanafunzi wetu wote wako salama kusoma na kufanikiwa katika majengo yetu ya shule. Tena, kwa kufuatilia mikakati mitano muhimu ya CDC ya kupunguza zaidi viwango vya hatari vya COVID-19 kama vile:

- Matumizi sahihi na ya mara kwa mara ya barakoa
- Kutokaribiana na watu ikiwa inawezekana
- Kunawa mikono
- Kusafisha na kuua vidudu
- Kuwafuatilia watu waliokaribiana kwa kushirikiana na Bodi ya Afya ya DeKalb

Tunawashukuru sana kwa ushirikiano wenu unaoendelea. Tutaendelea kuchunguza chaguo la kipimo cha COVID na kuendelea kujielimisha kuhusu nafasi za chanjo kwa wale ambao wanataka. Tafadhali jiunge nami mnamo Januari 16 saa 6pm kwa Mkutano wa Mtandaoni wa Town Hall. Unaweza kupata maelezo mapya kwenye tovuti yetu kwenye www.dekalbschoolsga.org.

Ninaendelea kujivunia kuwa sehemu ya jamii hii kuu. Ninaamini kwamba sisi ndio watu tunaofaa wa kufanya maamuzi sahihi kwa watoto wetu. Una ahadi yangu kwamba tutaendelea kwa umakini, kwa kimkakati, na kwa uwazi huku tukiweza kubadilika kwa urahisi kulingana na hali, kuwa wavumilivu, na wenye huruma.